*Kazi ya sasa ni tafsiri isiyo rasmi ambayo mchapishaji anakubali jukumu kamili. Chapisho hili lilitafsiriwa kwa uhuru na mashirika yafuatayo: Social Development Direct na Translators without Borders.*

Dondoo

# MKAKATI WA KIKANDA WA KIJAMII WA ASASI MBALIMBALI RUFAA YA MALALAMISHI KATIKA AMERIKA

Kwa rufaa za malalamishi yanayohusu Ukatili na Unyanyasaji wa Kijinsia (SEA)/ Uvamizi wa Kingono (SH) Kikanda za kuvuka mipaka za Asasi Mbalimbali

## 2.1 KANUNI ZA KUONGOZA NA VIWANGO VYA CHINI

Ili kuzuia na kulinda watu vya kutosha dhidi ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia, na dhuluma ya kijinsia, na wafanyakazi wake wowote, wahudumu wanaoshirikishwa wanajitolea kushirikiana kamili na kutoa usaidizi kwa kila mmoja kwa kufuata yafuatayo:

### MWENENDO WA WAFANYAKAZI

Wahudumu wote wanafaa kuridhia na kuendeleza ndani ya mashirika yao**Kanuni Kuu Sita Zifuatazokuhusiana na PSEA,** zilizochukuliwa kutoka **Kamati ya Kudumu ya Asasi Mbalimbali**(IASC/2002/ Imeboreshwa 2019) (Kiambatisho II). Hizi pia zimeelezwa kwenye *Taarifa Kuu ya Baraza la Usalama kuhusu Hatua Maalumu za ulinzi dhidi ya ukatili na dhuluma ya kijinsia*(ST/SGB/2003/13) (Kiambatisho I) na *Taarifa ya Umoja wa Mataifa kuhusu Kujitolea kwa Umoja wa Mataifa na Wafanyakazi wasio wa Umoja wa Mataifa* (2006) (Kiambatisho II):

1. Ukatili na unyanyasaji wa kijinsia na wafanyakazi wa misaada unajumuisha vitendo vya mwenendo mbaya na kwa hivyo ni sababu za kukomesha ajira.
2. Matendo ya ngono na watoto (watu walio chini ya umri wa miaka 18) ni marufuku bila kujali umri wa wengi au umri wa idhini katika eneo lako. Kukosa kujua umri wa mtoto hakutakusadia kujitetea.
3. Kubadilishana pesa, ajira, bidhaa, au huduma kwa ajili ya ngono, ikijumuisha upendeleo wa kingono au aina zingine za tabia za kudunisha, kuhujumu au unyonyaji zimepigwa marufuku. Hii inajumuisha kubadilishana misaada inayofaa kwa wafaidika.

*10.* Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa UNHCR: *http://www.unhcr.org/pages/52e11b746.html*
*11. https://oios.un.org/*
*12.* Taarifa ya Kujitolea ya UN, *https://cdu.unlb.org/Portals/0/PdfFiles/PolicyDock.pdf*

4. Uhusiano wowote wa kingono kati ya wale wanaotoa misaada ya kibinadamu na ulinzi na mtu anayefaidika na msaada huo wa kibinadamu na ulinzi ambao unahusisha utumiaji mbaya wa cheo au mamlaka ni umepigwa marufuku. Mahusiano kama hayo yanadunisha uaminifu na uadilifu wa kazi ya misaada ya kibinadamu.
5. Pale ambapo mfanyakazi wa kibinadamu anakua na wasiwasi au tuhuma kuhusu ukatili au unyonyaji wa kijinsia na mfanyakazi mwenzake, iwe katika shirika moja au la, lazima apige ripoti kuhusu wasiwasi kama huo kupitia mikakati iliyowekwa ya shirika za kupiga ripoti.
6. Wafanyakazi wa kibinadamu wanalazimika kuunda na kudumisha mazingira ambayo yanazuia unyonyaji na unyanyasaji wa kijinsia na kuendeleza utekelezaji wa maadili yao. Wasimamizi katika ngazi zote wana majukumu fulani ya kusaidia na kuunda mifumo inayodumisha mazingira haya.

Wafanyakazi wote wanafaa kuelea na kutia saini Kanuni za Maadili**ya Shirika,** au waraka kama huo **(tazama Kifaa cha Zana 10 – Mfano wa Kanuni ya Maadili ya PESA/SH na Zana11 - Mwongozo kuhusukuhusu Unyanyasaji wa Kijinsia)** unaoeleza viwango vinavyokubalika na visivyokubalika na kama vinavyoelezwa hapo juu. Wahudumu wote wanalazimika kuchukua hatua muhimu za kinidhamu kuzuia na kukabiliana na mwenendo mbaya wa wafanyakazi wao. Wahudumu wote wanapaswa kukabili kwa bidii wakati wowote visa vinapotokea kupitia kuanzisha na kuendesha kwa mikakati ya kupiga ripoti malalamishi katika jamii (kila mmoja au kwa pamoja na wahudumu wengine) na mkakati huu.

Wahudumu wanaoshiriki wanapaswa kujitolea **kukataa kabisa katika shirika** kisa chochote cha SEA / SH na kuchukua kwa uzito madai yote ya mwenendo mbaya.

## VIWANGO VYA CHINI NA KANUNI ZA MWONGOZO

Kuanzisha mfumo thabiti wa rufaa ya malalamishi, Mkakati huu unatambua umuhimu wa kufikia mazoea bora 13 ya[kimataifa] kuhusu PSEA na, kujumuisha Viwango vya Chini vya IASC vya Uendeshaji kwa PSEA (MOS PSEA) (Kiambatisho III).

Wahudumu wote wanaoshiriki wanakubali kufuata kanuni za **faragha, usiri, idhini kwa kufahamu, kutopendelea, heshima, usalama na ustawi** katika kutekeleza Mkakati na wakati madai au malalamishi yoyote yanapotolewa kwa shirika lao.

Mtazamo **unaojikita kwa mnusurika** unaongoza kukabili na uzuiaji wa PSEA / SH ambapo mnusurika anaarifiwa, anashiriki katika mchakato wa kufanya uamuzi kadiri inavyowezekana, na kutoa idhini kuhusu matumizi na ufichuzi wa habari.

Hofu ya athari kama vile kuondolewa kwa ulinzi, msaada au huduma, au hatari ya kubaguliwa zaidi, mara nyingi ni sababu kuu inayofanya watu wanaohusika na wafanyakazi hawawezi kupiga kuripoti visa vya PSEA / SH kwa shirika kuhusu wafanyakazi wake. Mnusura hafai kamwe kulaumiwa kwa SEA / SH. Wahudumu wanaoshiriki wanapaswa kuzingatia ustawi wa kisaikolojia wa mnusura wakati wa kuandaa mpango wa usalama / ulinzi, kwa kuzingatia kwamba manusura wa SEA wanaweza kutelekezwa kwa sababu ya imani za kitamaduni. Matendo na majibu ya wahudumu wote yataongozwa na **kuheshimu chaguzi, matakwa, haki, na utu wa mnusurika.**

13. Jopo kazi la PSEA, Mwongozo Matendo Bora Mwongozo wa Mikakati ya Malalamishi ya Asasi Mbalimbali ya PSEA (2019)
*http://www.pseataskforce.org/uploads/tools/1490964201.pdf*

Wahudumu wanapaswa kufanya kila juhudi kuhakikisha kuwa mhusika wa malalamishi hatangamani tena na mnusurika, kama vile kusitisha ajira kutoka kwa shirika husika au kwa hatua ya polisi ikiwa inafaa, kufuatia tathmini ya hatari na kwa kuzingatia sera ya rasilimali watu na kanuni za mchakato unaostahili. Huduma za ulinzi katika Kanda ya Amerika zinahitaji kuhusishwa kutoa huduma zao na msaada (kwa mfano RSSN) [14].

Wahudumu wote wanaoshiriki wanapaswa kushirikiana na kusaidiana katika kukabili na kuzuia SEA / SH pamoja na kufuata kanuni kuu zifuatazo zinazoongoza Mkakati huu:

- Kuendeleza ushirikiano na usaidizi kati ya mashirika katika kukabili na kuzuia SEA / SH
- Kuboresha usalama na ulinzi kwa watu wanaohusika, haswa katika maeneo ambayo hatari ya SEA ni kubwa **[Tazama Zana ya Kikanda: Zana 8 - Tathmini ya Hatari na Mikakati ya Uendeshaji na Programu Salama]**
- Fanya upigaji wa ripoti visa vya SEA /SH kuwa lazima (tazama sehemu ya 3 hapa chini)
- Mafunzo kuhusu uzuiaji wa SEA/SH yafanywe kuwa lazima kwa wafanyakazi wote wa mashirikayanayoshiriki**[Tazama Zana ya Kikanda: Zana 11 - Makala ya mafunzo ya PSEA / SH]**
- Kutekeleza uhakiki thabiti wa wafanyakazi wapya wa wahudumu wanaoshiriki
- Kuhakikisha ushiriki sawa na thabiti wa watu wanaohusika katika kutathmini, kupanga, kutekeleza, kufuatilia, na kuchambua msaada na huduma **[Tazama Zana ya Kikanda: Zana 2 – Mwongozo - Mashauriano na Wanaohusika]**
- Kwa kutambua kuwa SEA / SH imejikita katika tofauti za kijinsia na mamlaka yasiyo sawa, wahudumu wanaoshiriki wanapaswa kuhakikisha kuwa shughuli zinafanywa kwa njia inayozingatia jinsia na kwamba maoni na mitazamo ya wanawake, wanaume, wasichana na wavulana, wenyeji, watu wenye ulemavu, watu na mwelekeo tofauti wa kijinsia na kitambulisho cha kijinsia, na asili zingine mbalimbali zimezingatiwa vya kutosha [15].
- Kuhakikisha kuwa msaada na huduma zote zimeundwa kwa njia inayosawazisha kuheshimu utaratibu unaofaa na njia inayolenga matakwa ya mnusura, usalama, na ustawi zinasalia kuwa kipaumbele katika masuala na taratibu zote
- Kujumuisha na kuingiza PSEA / SH katika huduma na programu zote
- Kuhakikisha uwajibikaji katika ngazi zote za shirika na shughuli zake
- Kuhakikisha kuwa msaada kwa manusura wa SEA inatolewa kwa njia salama, inayoweza kupatikana na isiyo na ubaguzi.

*14.* Zana ya RSSN*https://www.acnur.org/5c05b97d4.pdf* na huduma ya RSSN ramani ya rufaa za SGBV/CP na hudumanyinginezo za ulinzi *https://www.arcgis.com/apps/MapSeries/index.html?appid=ae15aa2fe0c4469b83ea10f0925e8625*
*15.* Sera ya UNHCR kuhusu Umri, Jinsia na Utofauti 2018*https://www.unhcr.org/5aa13c0c7.pdf*

# KIAMBATISHO III

## VIWANGO VYA CHINI VYA ISASC VYA UENDESHAJI

## ULINZI DHIDI YA UNYONYAJI NA DHULUMA YA KIJINSIA KWA WAFANYAKAZI (MOS-PSEA)[1]

Ili kutoa ulinzi dhidi ya unyonyaji na unyanyasaji wa kijinsia (PSEA) na wafanyakazi wenyewe, kufuata viwango vya chini vya Uendeshaji wa PSEA (MOS-PSEA) kunahitajika. MOS-PSEA imeundwa kwa kufuata Viwango Maarufu vya Chini vya Usalama wa Uendeshaji kwa Usalama wa Wafanyakazi (au MOSS) Mkakati wa uzingatiaji ni lazima kwa Mfumo wa Umoja wa Mataifa kuhakikisha kuwa kuna seti ya mahitaji ambayo mashirika yote yanafuata ili kuhakikisha usalama wa wafanyakazi ..

### JE, MOS-PSEA NI NINI?

MOS-PSEA inajikita kwa:

1. Taarifa ya Kujitolea Kukomesha Unyonyaji na Unyanyasaji wa Kijinsia na Wafanyakazi wa Umoja wa Mataifa na wasio wa Umoja wa Mataifa, Agosti 2008
2. Ukaguzi wa Kiulimwengu wa ulinzi dhidi ya Unyonyaji na Unyanyasaji wa Kijinsia na Umoja wa Mataifa, Shirika lisilo la Kiserikali, IOM na Wafanyikazi wa IFRC, Julai 2010
3. Kanuni Kuu Sita za IASC zinazohusiana na Unyonyaji na Unyanyasaji wa Kijinsia, Juni 2002

### JE, ELEMENTI KUU ZA MOS-PSEA?

Nguzo nne za kazi ya PSEA ya sasa inatoa mfumo wa mkakati. Hizi ni:

1. **Usimamizi na uratibu:** Uundaji bora wa sera na utekelezaji; Mipango ya ushirika; Idara/mratibu wa kushughulika na PSEA.
2. **Kushirikiana na kusaidia jamii ya wenyeji:** Mawasiliano yenye upana nafanifu kutoka Makao Makuu kwenda nyanjani kuhusu (a) cha kufanya kuhusu kuimarisha uelewa wa wafaidika kuhusu PSEA na (b) jinsi ya kuanzisha mkakati mzuri wa malalamishi ya jamii.
3. **Kuzuia:** Mkakati mzuri na kamili wa kuhakikisha uhamasishaji kuhusu SEA miongoni mwa wafanyakazi; utaratibu mwafaka wa kuajiri na usimamizi wa utendakazi.
4. **Kukabili:** Taratibu za ndani za Malalamishi na uchunguzi zimewekwa.

1. MOS hizi zimejadiliwa miongoni mwa Wanachama wa Jopo Kazi ya IASC PSEA; hati hii ni kazi inayoendelea na inaonyesha hali ya mawazo ya sasa ya Jopo Kazi.

| VIWANGO VYA CHINI VYA UENDESHAJI WAPSEA | VIGEOZO VIKUU |
|---|---|
| **1. UUNDAJI BORA WA SERA NA UTEKELEZAJI** | • Sera inayoelezea viwango vya mwenendo, ikijumuisha vitendo vya SEA, vipo na mpango wa kazi wa kutekeleza sera uko tayari.<br>• Sera/viwango vya mwenendo vimewasilishwa kwa wafanyakazi wa sasa na wasimamizi wakuu (katika Makao Makuu na nyanjani) mara kwa mara (kama vile maelekezo na mafunzo ya ziada). |
| **2. MIPANGILIO YA USHIRIKIANO** | • Taarifa Maalumu ya Katibu Mkuu (ST / SGB / 2003/13) au kanuni za maadili zinazohusika zimejumuishwa katika masharti ya jumla ya kandarasi.<br>• Taratibu zipo za kupokea makubaliano ya maandishi kutoka kwa mashirika au watu wanaokubaliana kushirikiana na shirika kwamba wanajua na watafuata viwango vya sera ya PSEA. |
| **3. MRATIBU/MKUU WA IDARA ANAYESHUGHULIKA NA PSEA** | • Mratibu/mkuu wa idara anayehusika anajukumu la jumla kwa uundaji na utekelezaji wa sera na shughuli za PSEA.<br>• Idara husika/mratibu anahitajika kupiga ripoti mara kwa mara kwa wasimamizi wakuu kuhusu hatua zinazopigwa kwa PSEA kupitia Mratibu Mkuu kuhusu PSEA.<br>• Wafanyakazi wanaoshughulikia PSEA wamepatiwa jukumu rasmi la PSEA katika maelezo yao ya kazi, tathmini ya utendakazi au taratibu kama hiyo.<br>• Wamepokea mafunzo yaliyopangwa ya PSEA na uliotengewa PSEA unatoshana na kiwango cha utekelezaji kinachohitajika chini ya hali ya sasa ya shirika. |
| **4. MAWASILIANO KAMILI YANAYOFAA KUTOKA MAKAO MAKUU KWENDA NYANJANIJUU YA MATARAJIO KUHUSU KUBORESHA UELEWA WA WAFAIDIKAKUHUSU PSEA** | • Makao Makuu yamewasilisha kwa kina matarajio kuhusu juhudi za uhamasishaji wafaidika kuhusu PSEA (ikijumuisha habari juu ya viwango vya mwenendo wa shirika na utaratibu wa kupiga ripoti).<br>• Makao makuu yamesambaza mifano ya zana za kuboresha uelewa na makala ya kutumiwa kwa shughuli za kuboresha uelewa wa wafaidika. |

| | |
|---|---|
| **5. MIKAKATI BORA YA MALALAMISHI YA JAMII (CBCM), IKIJUMUISHA MSAADA KWA WAHASIRIWA** | • Makao Makuu yanahimiza ofisi zake za nyanjani kushiriki katika mikakati ya malalamishi ya jamii ambayo yaliundwa kwa pamoja na kutekelezwa na jamii ya kutoa misaada na kuhawilishwa kwa maeneo maalumu.<br>• Kuna mwongozo uliotolewa nyanjani kuhusu jinsi ya kubuni CBCM kuhakikisha inaingiliana na muktadha wa kitamaduni kwa kulenga ushiriki wa jamii.<br>• Kuna mkakati wa ufuatiliaji na uhakiki wa mkakati wa malalamilishi.<br>• Shirika limeandika mwongozo kuhusu utoaji wa msaada kwa wahasiriwa. |

| VIWANGO VYA CHINI VYA UENDESHAJI WAPSEA | VIGEOZO VIKUU |
|---|---|
| **6. UTARATIBU BORA WA KUAJIRI NA USIMAMIZI WA UTENDAKAZI** | • Shirika linahakikisha kuwa wagombea wote wanatakiwa kusaini kanuni za maadili kabla ya kupewa kandarasi.<br>• Kila shirika linaahidi kuboresha mfumo wake wa kukagua marejeleo na kukagua mwenendo mbaya wa zamani.<br>• Usimamizi na tathmini ya utendakazi inajumuisha kufuatilia ushiriki katika mafunzo ya Kanuni ya Maadili (au sawa) inayojumuisha PSEA.<br>• Tathmini ya utendakazi wa Wasimamizi Wakuu inajumuisha kufuata ili kuunda na kudumisha mazingira yanayozuia unyonyaji na unyanyasaji wa kijinsia na inakuza utekelezaji wa ST/ SGB / 2003/13 au kanuni za maadili. |
| **7. MIKAKATI BORA NA KAMILI ZIMEWEKWA ILI KUHAKIKISHA UBORESHAJI WA UELEWA KUHUSU SEA MIONGONI MWA WAFANYAKAZI** | • Wafanyakazi wanapokea mafunzo ya ziada kila mwaka kuhusu viwango vya mwenendo, wanajifunza kuhusu mikakati ya kuwasilisha malalamishi ripoti za mwenendo mbaya na athari za kukiuka viwango hivi.<br>• Mafunzo kuhusu mwenendo mbaya (haswa kutaja SEA) ni sehemu ya mchakato wa maelekezo.<br>• Wafanyakazi wanajua wajibu wao wa kupiga ripoti visa vya SEA/mwendendo mbaya na wanajua kuwa kuna sera ya Ulinzi dhidi ya kulipiza kisasi. |
| **8. TARATIBU ZA NDANI ZA MALALAMISHI ZILIZOPO** | • Taratibu zilizoandikwa kuhusu kushughulikia malalamishi/ripoti kutoka kwa wafanyakazi au wafaidika zipo.<br>• Wafanyakazi wanajulishwa mara kwa mara kuhusu jinsi ya kuwasilisha malalamishi/ripoti na taratibu za kuzishughulikia.<br>• Taratibu za kawaida za uendeshaji wa uchunguzi au zilizo sawa na hizo na zinatumika kuongoza uchunguzi.<br>• Uchunguzi unafanywa na wataalamu wenye ujuzi na walio na uzoefu ambao pia wamefundishwa kuhusu uchunguzi nyeti kama vile madai ya SEA.<br>• Uchunguzi unaanzishwa ndani ya miezi 3 na habarikuhusu matokeo yanakabidhiwa mlalamishi.<br>• Malalamishi yaliyothibitishwa yamesababisha hatua za kinidhamu au kuathiri kandarasi na, ikiwa sio hivyo, shirika linaweza kuhalalisha uamuzi wake. |